JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

IFAHAMU TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Juni, 2007

Imetolewa na:
Katibu, Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Umma
S.L.P. 9143, Dar es Salaam.

DIBAJI

Tume ya Utumishi wa Umma ina jukumu la kuhakikisha kuwa usimamizi wa rasilimali watu unainufaisha sekta ya Utumishi wa Umma kwa kufanikisha upatikanaji wa huduma bora na sahihi. Utekelezaji wa jukumu hili unafanyika kama ifuatavyo:

- Kufanya ukaguzi katika mamlaka za ajira na nidhamu ili kuona kama mamlaka hizo zinazingatia sheria, kanuni, taratibu, miongozo na nyaraka mbali mbali zinazotolewa na serikali katika kuajiri na kuchukua hatua za kinidhamu katika utumishi wa umma
- Kuandaa na kutoa miongozo kuhusu masuala ya ajira na nidhamu kwa ajili ya mamlaka za ajira na nidhamu ili kuwezesha utekelezaji wa masuala ya ajira na nidhamu
- Kutoa maamuzi ya haki na usawa juu ya rufaa zinazowasilishwa Tume kupinga maamuzi ya kinidhamu yaliyofikiwa na mamlaka za nidhamu katika utumishi wa umma.
- Kutoa mafunzo na ufafanuzi wa miongozo inayotolewa na Tume kwa mamlaka za ajira na nidhamu na wadau wengine wa Tume

- Kushiriki katika kamati za ajira ili kuhakikisha kuwa taratibu na kanuni zinazohusu ajira zinatekelezwa ipasavyo.

Ili kazi hii iweze kufanikiwa na kuwezesha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi Tume inajenga na kuimarisha uelewa wa sheria, kanuni na taratibu zake kwa kutumia mbinu mbali mbali ili mamlaka za ajira na nidhamu ziweze kuzingatia kikamilifu sheria, kanuni na taratibu zake katika kusimamia rasilimali watu. Miongoni mwa mbinu hizo ni pamoja na vipeperushi, majarida, semina na vijitabu. Kwa mara hii Tume imeandaa Kijitabu "Ifahamu Tume ya Utumishi wa Umma" ambacho kinaelezea kwa kifupi mambo ya msingi ya Tume kama vile kuanzishwa na majukumu yake, sifa kama jambo la msingi katika ajira yoyote, uzingatiaji wa kanuni na taratibu katika utekelezaji wa masuala ya nidhamu na rufaa katika utumishi wa umma. Kijitabu hiki kimeelezea mambo hayo kwa kutumia viponzo ili kujenga mazingira ya kumrahisishia msomaji kupata ujumbe au uelewa.

1.0 KUANZISHWA KWA TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Tume ya Utumishi wa Umma ni Idara ya Serikali inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais. Ilianzishwa kwa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002. Tume iliundwa ili kuboresha Utumishi wa Umma kwa kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma ni mmoja na kuwa watumishi wote wana taratibu za usimamizi, hadhi, haki na maslahi yanayofanana. Jukumu la Tume ya Utumishi wa Umma ni kuhakikisha kuwa masuala yote ya



kiutumishi yanaendeshwa kwa haki na usawa na yanalenga katika utendaji wenye malengo maalum.

2.0 DIRA NA DHAMIRI YA TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Dira ya Tume ni **Kuwa mfano wa kuigwa katika Afrika kwa kuhimiza masuala ya ubora, uwajibikaji na uadilifu katika Utumishi wa Umma.**



Aidha, **Dhamiri** ya Tume ni **Kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unatoa huduma bora kwa Watanzania kwa kuwezesha, kufuatilia na kutathimini shughuli za Usimamizi wa Rasilimali watu unaozingatia sifa na uwezo na kushughulikia rufaa na malalamiko kwa kuwatumia watumishi wenye uwezo mzuri kitaaluma.**

3.0 MUUNDO WA TUME

Muundo wa Tume ya Utumishi wa Umma utakuwa kama ifuatavyo:

3.1 Wajumbe

Kwa mujibu wa kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kinaelezea kuhusu kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Umma ambayo itaundwa na Mwenyekiti na wajumbe wasiozidi 6 ambao watateuliwa na Rais. Aidha kwa mujibu wa kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Tume itakuwa na Katibu ambaye pia atateuliwa na Rais. Katibu ndiye Mtendaji Mkuu na Afisa Mhasibu.

3.2 Idara

Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kifungu cha 15(1) Tume ina Idara tano (5) ambazo zinaongozwa na Manaibu Katibu. Idara hizo ni:-

- Idara ya Utumishi wa Afya.
- Idara ya Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji.
- Idara ya Utumishi wa Serikali za Mitaa.
- Idara ya Utumishi Serikalini.
- Idara ya Utumishi wa Walimu. Idara hii ina ofisi za Mikoa na Wilaya

3.3 Kurugenzi ya Utawala na Utumishi

Kurugenzi hii ambayo inaongozwa na Mkurugenzi, ina vitengo vya Uhasibu, Ukaguzi wa Ndani, Sheria, Habari na Teknolojia, Habari na Mawasiliano.

4.0 MAJUKUMU YA TUME

- Kuhakikisha kuwa Taratibu za Uendeshaji za Utumishi wa makundi mbalimbali zinatayarishwa na kutumika ipasavyo;
- Kuandaa na kupitia miongozo kuhusu sifa zitakazotumika katika masuala ya ajira na upandishaji vyeo;
- Kuzisaidia Mamlaka za Ajira katika kufanikisha tathmini

zitokanazo na utendaji;

- Kupokea na kushughulikia rufaa za mashauri yaliyotolewa maamuzi na Mamlaka za Nidhamu isipokuwa Mamlaka ya Katibu Mkuu Kiongozi;
- Kushughulikia ajira, upandishaji vyeo, nidhamu na usajili wa walimu;
- Kuwezesha, kufuatilia na kutathmini utendaji kazi wenye kuzingatia matokeo katika Utumishi wa Umma.

5.0 AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

5.1 Ajira

Ajira katika Utumishi wa Umma itazingatia sifa, haitakuwa na upendeleo, ukabila, udini wala rushwa.

5.2 Kupandishwa cheo

Utaratibu wa kupandisha cheo katika Utumishi wa Umma utazingatia

- Sifa
- Nafasi wazi ya kazi
- Uwepo wa fedha za kulipa mishahara
- Utendaji bora wa kazi



6.0 NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

6.1 Taratibu katika kuendesha mashauri ya nidhamu

Katika kuendesha mashauri ya nidhamu, mamlaka za nidhamu zinapaswa kuzingatia taratibu zifuatazo:

- Kufanya uchunguzi wa awali ili kubaini iwapo kuna haja ya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtumishi
- Kutoa notisi na hati ya mashtaka iliyosainiwa na mamlaka ya nidhamu

- Kuunda kamati ya uchunguzi endapo mtumishi hajakiri kosa.
- Kutoa uamuzi wa shauri ndani ya siku 30 baada ya kupokea taarifa ya kamati ya uchunguzi
- Kumjulisha mtumishi haki yake, muda na mahali pa kukata rufaa.

7.0 RUFAA

7.1 Mamlaka za rufaa

Mtumishi anayo haki ya kukata rufaa kwa mamlaka husika



ya rufaa. Hali kadhalika mamlaka ya nidhamu ina haki pia ya kukata rufaa kwa mamlaka husika ya rufaa kama ifuatavyo:-

i) **Rais**

Rais ni mamlaka ya rufaa kwa uamuzi wa Tume ya Utumishi wa Umma na wa Katibu Mkuu Kiongozi.

ii) **Tume ya Utumishi wa Umma**

Kwa upande wa watumishi ambao mamlaka zao za nidhamu ni Waziri Mwenye Dhamana ya Serkali za Mitaa, Katibu Mkuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mkuu wa Idara inayojitegemea, Katibu Tawala wa Mkoa, Mkurugenzi wa Uhamiaji au Kamishna wa Zimamoto na Uokoaji, watakata rufaa zao Tume ya Utumishi wa Umma.

iii) **Walimu**

Kwa upande wa walimu mamlaka za rufaa zitakuwa kama ifuatavyo:

- Kamati ya Wilaya kwa uamuzi uliofanywa na Mkuu wa Shule au Chuo

- Kamati ya Mkoa kwa Uamuzi uliofanywa na kamati ya Wilaya
- Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD) Makao Makuu kwa uamuzi wa Kamati ya Mkoa
- Tume ya Utumishi wa Umma kwa uamuzi uliofanywa na Idara ya Utumishi wa Walimu
- Rais kwa uamuzi uliofanywa na Tume ya Utumishi wa Umma

iv) **Watumishi wa Kawaida (Operational Service)**

Kwa upande wa watumishi wa kawaida, utaratibu wao wa kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa mamlaka zao za nidhamu utazingatia Sheria ya Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004.

7.2 Taratibu za kukata rufaa

Endapo mtumishi ataona hakutendewa haki na mamlaka yake ya nidhamu basi atakata rufaa kwa mamlaka ya rufaa inayohusika katika kipindi kisichozidi siku 45 tangu apokee

barua ya uamuzi na kupeleka nakala ya rufaa yake kwa mamlaka yake ya nidhamu.

Tume ya Utumishi wa Umma
Jengo la Acasia, Mtaa wa Samora,
S.L.P. 9143 Dar es Salaam
Simu: +255 (22) 2126811/4, 2126260
Faksi: +255 (22) 2114158